



TIST HABARI MOTOMOTO JULY 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Photo 1: Ibwaga Cluster Meeting

In this newsletter, we are going to have;

- I. Cluster Best Practices
- II. Baseline for New Small Group
- III. Planting Trees for TIST

(I) Cluster Best Practice

- Your Small Group members should attend Cluster Trainings every month
-
- At the Cluster meeting, Cluster Servants and Cluster Leaders should work together to provide
- TIST members with high Quality Trainings, provide them with latest TIST News and Information,
- Answer their Questions, Concern and or Grievances. They should also communicate with
- TIST Leadership on any requests Cluster members may have.
- Cluster Servants and Cluster Leaders may use Training Materials provided in TIST Mobile website, TIST Learning Center, Printed Training Materials, TIST Chatbox, Habari Moto Moto Newsletter and Seminar Notes.
- Cluster Servant should use pendragon forms to give Cluster meeting and Accounting Reports and make sure they synchronize that information to the TIST Database.
- Additionally, Cluster Servants should update in the TIST Mobile Website, the Cluster meeting dates, dates of election and Cluster Leaders information
- **Why Do We Work in Clusters?**
- 1. To keep costs of serving TIST Small Groups low so that more carbon money goes to farmers.
- 2. To allow Small Groups to serve themselves more easily.
- 3. To allow TIST to expand more quickly by partnering with organizations who want to join TIST.

What Does a Good Cluster Look Like?

- A Cluster should have 30-50 Small Groups.
- A Cluster's Small Groups should be within walking distance of a central meeting point.
- A Cluster Servant should do an accurate quantification and high quality training for a Cluster.
- A Cluster may establish seedlings in nurseries for annual planting needs.
- A Cluster should also ensure individual TIST Farmers are encouraged to raise seedlings on their own farms.

TIST Small Groups Plant 'the right number' of trees around your houses, along fence lines, mixed with crops in your farm, etc.

What Should a Good Cluster Do?

A Cluster should hold elections each 4 months to select an Accountability Person who will rotate through the positions.

A Cluster should meet every month for training, sharing of best practices, distribution of Habari Moto Moto Newsletter, payments, and other matters.

Cluster Servants and Leaders should welcome new members at the Cluster meeting

Cluster Servant should each month make arrangements with Small Groups members that will have their trees quantified till the next Cluster meeting

Cluster Servant should at every Cluster Meeting notify each Small Group their current status
- Profit share eligibility, number of Groves and trees Quantified etc.

TIST HABARI MOTO MOTO

(II) Baseline for New Small Group

Your Small Group members should identify areas they want to plant trees now and in future

Your Small Group members should be present when a Cluster Servants come to take Baseline (To answer Questions related to ownership, history of the land etc.)

Baseline yields to getting the Grove into a PDD (Project Design Document). This is the first step in participating in carbon credit business

Baseline involves answering questions about the Grove area a farmer has identified for planting trees

- Ownership (Please show a Title Deed, Permission from land owner, Customary Lease or any document that allow you to plant/own the land) (If no ownership proved, Grove cannot Qualify)
- Forest. Whether a Grove is already a Forest (If Yes, the Grove cannot Qualify)
- Deforested (Last 10 years). If yes, Grove cannot qualify
- Displacement. If a farmer is stopping other activities so as to plant trees for carbon, this Grove cannot qualify

Topography

- Baseline Trees and baselines Stumps (Baseline trees and trees that sprout from Baseline stumps are not quantified as TIST Trees)
- Tracks – Primary track 1 and track 2.

Your Cluster Servant will only take track when satisfied your Grove meets all Baselines Requirements

Your Cluster Servant will also take GPS Readings at the center of the Grove.

(III) Planting Trees for TIST

- A Farmer should Plant trees following TIST Best Practices
- To assure higher survival of your trees, plant trees on the onset of rains.
- Remind yourself and other members in your Small Group to use 2m Tree spacing or 3-4m for fruit and nut trees.
- You are encouraged to plant different species of trees – mix indigenous, exotic, fruit, fodder and nut trees
- Always weed your Groves and water your trees during dry season.
- Farmers should plant trees that can last 60 years and more.
- Remember, Trees are Quantified when they have been Transplanted in the Grove area and are 6 months and older
- Trees that harm the environment or soil are not encourage
- No trees should be planted in wetlands – TIST doesn't count trees planted in wetlands.
- Eucalyptus are not counted as TIST trees



Photo 2: One of the TIST Farmer Groves

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST Values

As TIST Family we have our Values which most of TIST Small Groups know and practice. We always reflect on these Values and to ensure that we all are truly living by them. The success of TIST is based on the integrity and effort of individual members within TIST. What we can achieve depends on each of us following these Values;

Who are we?

- (i) We are Honest
- (ii) We are Accurate
- (iii) We are Transparent
- (iv) We are Servants to each other
- (v) We are Mutually Accountable to Each Other and
- (vi) We create Low Budget/ cost, yet we achieve Big Results

How we do things that other people can see

- 1) We are committed
- 2) We do our work in small groups
- 3) We seek and use the best way
- 4) We use our minds and hands.

What do we do?

- 1) We plant different species of trees for long -term
- 2) We find ways to improve our health
- 3) We practice Conservation Farming
- 4) We do other projects and businesses (sustainable agriculture, nurseries, citrus growing, dairy goats and farming, chickens, bee keeping, fishponds and fish keeping, silkworm farming etc.)
- 5) We sell carbon credits

What do we create?

- 1) We create team work - by doing things this way; we end up working as a team.
- 2) We create capacity - we create organization, strength, and a system that is strong.
- 3) We create enjoyment - we see results, we accomplish big things that we enjoy.
- 4) We create Big Results - In Conservation Farming and from other projects and business that we do.
- 5) We create Low Budget/Cost, yet we achieve big results.



TIST HABARI MOTOMOTO JULY 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Picha: Klasta ya Ibwaga

Katika jarida hili, tutakuwa na:

- (I) Kutambua Mbinu Bora za Klasta
- (II) Kuchukua taarifa za awali za Kikundi Kidogo Kipya (kufanya Baseline)
- (III) Kupanda Miti kwa ajili ya TIST

TIST HABARI MOTO MOTO

Kutambua Mbinu Bora za Klasta

Kikundi chenu Kidogo mnapaswa kuhudhuria Mafunzo na Mikutano ya Klasta kila mwezi

Kwenye Mkutano wa Klasta, Watumishi na Viongozi wa Klasta wanapaswa kufanya kazi pamoja ili kutoa Mafunzo bora kwa Wanachama wa TIST na kuwapatia taarifa na habari mpya za TIST.

Viongozi na watumishi wa Klasta wanapaswa kujibu Maswali, Wasiwasi na au Malalamiko yao na pia kuwasiliana na Uongozi wa TIST kwa maombi yoyote ambayo wanachama wa Klasta wanaweza kuwa nao.

Watumishi na Viongozi wa Klasta wanaweza kutumia Mafunzo yanayopatikana kwenye tovuti ya TIST, Kituo cha Mafunzo cha TIST, vitini vilivyochapishwa kwa ajili ya Mafunzo, TIST Chatbox, Jarida la Habari Moto Moto na Vidokezo vya Semina.

Mtumishi wa Klasta anapaswa kutumia fomu za pendragon kutoa taarifa za Mkutano wa Klasta na mahesabu na kuhakikisha kuwa wanaingiza taarifa hizo kwenye mtandao wa TIST.

Pia, Watumishi wa Klasta wanapaswa kuweka taarifa za viongozi wa Klasta, tarehe za mafunzo, uchaguzi na tarehe za mikutano kwenye mtandao wa TIST

Kwa Nini Tunafanya Kazi Katika Vikundi?

1. Ili kuweza kuhudumia Vikundi Vidogo vya TIST kwa gharama nafuu na kuwezesha pesa nyingi za kaboni ziende kwa wakulima.

2. Kuruhusu Vikundi Vidogo kujihudumia kwa urahisi zaidi.

Klasta Nzuri Inaonekanaje?

-Klasta inapaswa kuwa na Vikundi Vidogo 30-50.

-Vikundi Vidogo vya Klasta vinapaswa kuwa ndani ya umbali wa kutembea kwa miguu kutoka sehemu kuu ya mkutano.

-Mtumishi wa Klasta anapaswa kufanya kazi ya kuhesabu miti (quantification) kwa usahihi na mafunzo ya hali ya juu kwenye Klasta.

-Klasta inashauriwa kuanzisha vitalu na kuotesha miche ya kutosha kwa mahitaji ya upandaji miti kila mwaka.

-Klasta inatakiwa kuhamasisha kila Kikundi kuwa na kitalu cha miche kwa ajili ya kupanda miti msimu unaofuata.

Vikundi Vidogo vya TIST vinatakiwa kupanda 'idadi sahihi' ya miti kuzunguka nyumba zao, kando ya uzio wa nyumba na shambani mwao wakichanganya miti na mazao, n.k.

Je! Klasta Nzuri Ifanye Nini?

Klasta inapaswa kufanya uchaguzi kila baada ya miezi 4 ili kuchagua Mtu wa Uwajibikaji ambaye atazunguka kupitia nyadhifa hizo.

Klasta inapaswa kukutana kila mwezi kushiriki mbinu bora, ugawaji wa Jarida la Habari Moto Moto, malipo, na mambo mengine.

Kuchukua majukumu ya kufundisha Klasta nyingine

TIST HABARI MOTO MOTO

Kuchukua taarifa za awali za Kikundi Kidogo Kipya (kufanya Baseline)

- Wanakikundi wanapaswa kutambua maeneo wanayotaka kupanda miti sasa na siku zijazo.
- Washiriki wa Kikundi wanapaswa kuwepo wakati Watumishi wa Klasta wanapokuja kuchukua taarifa za awali (ili kujibu maswali yanayohusiana na umiliki, historia ya ardhi n.k)
- Matokeo ya taarifa za awali za shamba zitasaidia kupata Hati ya Usanifu wa Mradi. Hii ni hatua ya kwanza katika kushiriki kwenye biashara ya kaboni
- Taarifa za awali zinahusisha kujibu maswali kuhusu eneo la shamba ambalo mkulima ametenga kwa ajili ya kupanda miti.
- Umiliki (Tafadhali onyesha Hati miliki, Ruhusa kutoka kwa mmiliki wa ardhi, umiliki wa Kimila au hati yoyote inayokuruhusu kupanda/kumiliki ardhi) (Ikiwa hakuna umiliki uliothibitishwa, shamba haiwezi kuwa na vigezo vya kupanda miti ya TIST)
- Miti ya awali na Visiki vya awali (Miti ya awali na miti inayochipuka kutoka kwenye visiki vya awali haitatambuliwa kama Miti ya TIST)
- Mzunguko wa shamba – Mzunguko wa 1 na wa 2. (Trucks) Mtumishi wako wa Klasta atachukua taarifa za shamba lako endapo tu limekidhi vigezo vyote wakati wa kuchukua taarifa za awali.
- Ikiwa eneo lilikuwa na msitu au kichaka (haliwezi kuwa na vigezo kupanda miti ya TIST)
- Ikiwa shamba ilikatwa miti (Miaka 10 iliyopita) shamba haiwezi kufuzu vigezo vya TIST
- Ikiwa mkulima anasimamisha shughuli zingine au kuhamisha watu ili kupanda miti ya kaboni, shamba hii haiwezi kufuzu vigezo vya TIST
- Mtumishi wako wa Klasta atafuatilia na kujiridhisha kuwa shamba lako imetimiza Masharti yote ya Msingi
- Mtumishi wako wa Klasta pia atachukua vipimo ya GPS katikati ya Grove
- Ikiwa shamba halistahiki, Mtumishi wa Klasta anapaswa kukujulisha sababu za kutostahiki

Kupanda Miti kwa ajili ya TIST

- Mkulima unashauriwa kupanda miti kwa kufuata Mbinu Bora za TIST
- Ili kuhakikisha miti yako inakuwa hai, panda miti mwanzo wa msimu wa mvua.
- Jikumbushe mwenyewe na wanachama wenzako katika Kikundi chenu kutumia vipimo vilivyopendekezwa. Umbali wa mita 2 au zaidi kwa miti ya matunda na miti ya karanga.
- Unahimizwa kupanda aina mbalimbali za miti - changanya miti ya kiasili, kigeni, matunda, malisho na ya jamii ya kokwa
- Palilia shamba lako kila wakati na kumwagilia miti yako wakati wa kiangazi.
- Wakulima wote tunakumbushwa kupanda miti ambayo inaweza kudumu miaka 60 na zaidi.
- Kumbuka, Miti huanza kuhesabiwa ndani ya kipindi cha miezi 6 au zaidi tangu inapokuwa imepandikizwa kwenye shamba lako (Grove)
- Haishauriwi kupanda miti inayoharibu mazingira au udongo
- Miti ya TIST haipaswi kupandwa katika maeneo ya kando kando ya vyanzo vya maji - TIST haitahesabu miti iliyopandwa katika maeneo hayo.
- Miti ya Mikaratusi haihesabiwi kama miti ya TIST



Picha: Moja ya shamba la Mkulima wa TIST

TIST HABARI MOTO MOTO

MAADILI YA TIST

Kama Familia ya TIST tuna Maadili yetu ambayo wengi wa Wanavikundi Vidogo vya TIST wanayajua na kuyatekeleza. Daima tunatafakari juu ya Maadili haya na kuhakikisha kwamba sote tunaishi kulingana nayo. Mafanikio ya TIST yanatokana na uadilifu na juhudi za wanachama binafsi ndani ya TIST. Tunachoweza kufikia inategemea kila mmoja wetu kufuata Maadili haya;

Sisi ni Nani?

- 1) Sisi ni waaminifu.
- 2) Sisi tunatoa taarifa sahihi.
- 3) Sisi ni wawazi
- 4) Sisi tunatumikiana.
- 5) Sisi ni wawajibikaji
- 6) Bajeti Ndogo, Matokeo Makubwa

Jinsi tunavyofanya mambo ambayo watu wengine wanaweza kuona

- 1) Sisi tunajitolea.
- 2) Tunafanya kazi zetu katika vikundi vidogovidogo
- 3) Tunatafuta na kutumia njia bora
- 4) Tunatumia akili na mikono yetu.

Tunachofanya

- 1) Tunapanda aina mbalimbali za miti itakayodumu kwa muda mrefu.
- 2) Tunafanya mambo kuboresha afya zetu.
- 3) Tunafanya Kilimo Hai.
- 4) Tunafanya miradi na biashara zingine.
- 5) Tunafanya biashara ya hewa ya kaboni.

Tunafanya.

- 1) Tunaunda kazi ya timu—kwa kufanya mambo kwa njia hii; tunaishia kufanya kazi kama timu.
- 2) Tunajenga Uwezo-tunaunda shirika, nguvu, na mfumo ambao ni imara.
- 3) Tunafanya mambo yanayotufurahisha-tunaona matokeo, tunatimiza mambo makubwa ambayo tunafurahia
- 4) Tunafanya mambo yanayoleta matokeo makubwa-matokeo makubwa ya upandaji miti. matokeo makubwa katika Kilimo Hai na matokeo makubwa kutokana na miradi na biashara zingine tunazofanya.
- 5) Tunatumia gharama ndogo za Utawala, lakini tunapata matokeo makubwa.